BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI NA MOJA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Tatu – Tarehe 27 Novemba, 2026

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Fedha:

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Chuo cha Fedha Zanzibar, Kuweka Masharti ya Utoaji wa Elimu katika Fani za Biashara na Fedha na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti Kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Chuo cha Fedha Zanzibar, Kuweka Masharti ya Utoaji wa Elimu katika Fani za Biashara na Fedha na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

II. MASWALI:

1. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Swali Nam.152: MHESHIMIWA MMANGA MOHAMMED HAMED (JIMBO LA TUMBE) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Pamoja na sifa nyingi zilizotolewa kwa Serikali kwa kuwajali wazee wetu ikiwa ni pamoja na kuwapa Pencheni Jamii kwa kila mwezi, juhudi hizi za Serikali zinakosekana kwa watu wenye ulemavu.

Kwa nini Watu wenye Ulemavu hawasaidiwi kila mwezi kama wanavyosaidiwa wazee.

2. Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Swali Nam. 127: MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (JIMBO LA OLE) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kwa kuwa siku ya Ijumaa ni siku muhimu sana kwa Waislamu, Ofisi nyingi za Serikali husitisha kutoa huduma kuanzia saa tano asubuhi hadi saa nane mchana.

Je, kuna muongozo wowote wa Serikali wa utoaji wa huduma kwa taasisi za Umma kwa siku hii ya Ijumaa.

Swali Nam. 147: **MHESHIMIWA SEIF HAMAD SULEIMAN (JIMBO LA OLE)-** Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria,Utumishi na Utawala Bora:

Kufuatia mabadiliko ya mishahara yaliyofanywa na Serikali hivi karibuni, yapo malalamiko mengi ambayo yanaonesha kutokuwepo kwa uwiano baina ya mfanyakazi mmoja na mwengine. Kwa mfano, mtu ambae ameajiriwa siku moja, fani moja na kiwango kimoja cha elimu, kuwa na ongezeko la mishahara tofauti na mwenzake kama yeye.

(a) Ni utaratibu gani uliotumika katika ongezeko hili la mishahara.

(b) Je, ni vigezo gani vinavyotumika kutafautisha mishahara katika Taasisi moja na nyengine, hali ya kuwa watumishi hawa huwa sawa kielimu na utaalamu.

3. Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

Swali Nam.70: **MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (NAFASI ZA WANAWAKE) -** Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Pamoja na kuwepo kwa ada za usafirishaji wa magari ya mizigo yanayobeba mchanga, wamiliki na madereva wa magari hayo hutozwa faini mbalimbali kwa kushusha mchanga barabarani, kuelemewa na tozo mbalimbali kupitia Halmashauri na hata faini za kuchukua rasilimali ya mchanga na nyengine katika muda ambao hauruhusiwi, pamoja na kuelemewa na faini zilizotangazwa hivi karibuni kwa Unguja na Pemba.

Je, ni vigezo vipi vilivyotumiwa na Wizara yako katika uwekaji wa ada za usafirishaji na kuwatoza faini na tozo mbalimbali wamiliki na madereva wa magari ya mchanga, kokoto, matofali na madini mengine yanayohusika.

4. <u>Wizara ya Afya:</u>

Swali Nam.124: MHESHIMIWA FARIDA AMOUR MOHAMMED (NAFASI ZA WANAWAKE) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa Hospitali ya Lumumba inapokea wagonjwa wengi kutoka maeneo tofauti ya visiwa vya Unguja na Pemba. Na kwa kuwa wananchi wengi wasiokuwa na uwezo, wenye wagonjwa wao katika hospitali hiyo, hubaki katika maeneo ya pembeni hospitalini hapo, kusubiri matokeo ya wagonjwa wao. Na kwa kuwa watu hao hukosa maeneo yenye huduma muhimu kama banda la kutosha kwa hifadhi yao, nguo na sehemu ya maji salama, ukiacha msikiti uliopo pembeni hapo.

(a) Kwa kiasi gani Serikali inalitambua tatizo hili liliopo katika hospitali hiyo.

(b) Lini Serikali itafikiria kujenga banda lenye hadhi la kuwastiri walipa kodi wake, walio wanyonge wenye wagonjwa wao katika hospitali ya Lumumba.

5. <u>Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi:</u>

Swali Nam. 17: MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (JIMBO LA PAJE) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Kumekuwa na mtindo kwa Bodi ya Wakadiriaji Majengo Zanzibar kuchelewesha vibali vya ujenzi mara baada ya waombaji kukamilisha taratibu katika Bodi ya Usajili wa Wakandarasi ambapo wakati mwengine vibali hivyo huwa havitolewi kabisa.

(a) Je, Bodi ya Wakadiriaji wa Majengo inafanya kazi kwa sheria au kwa matakwa ya watu binafsi mpaka inafikia maamuzi ya kutotoa vibali au kuchelewesha.

(b) Kwa nini utaratibu wa kutoa vibali kwanini usifanyike kwa njia za wazi kama mwombaji ameshakamilisha hatua muhimu zinazotakiwa kisheria.

(c) Endapo kibali kinacheleweshwa bila kutolewa sababu za msingi na kwa kuzingatia muda, je, Bodi itawekewa utaratibu gani wa kutoa fidia kwa waombaji wanaoathirika.

Swali Nam. 51: MHESHIMIWA MOHAMMED ALI SALIM (JIMBO LA ZIWANI) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Kwa muda mrefu sasa wananchi wanaizungumzia Barabara ya Chake-Mkoani kwa ubovu wake huku wakiendelea kuwa na matumaini ya ujenzi wake wa haraka.

Ni lini Serikali imekusudia kuanza ujenzi wa barabara hiyo hasa ikizingatiwa kuwa ndio uti wa mgongo wa uchumi wa shughuli zote muhimu za kiuchumi za kisiwa cha Pemba.

Swali Nam.160: MHESHIMIWA SHAFI MOHAMMED SHAFI (JIMBO LA WETE) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Katika Mkutano wa Bajeti kwa mwaka 2026/2027, Serikali ilituambia kuwa, kuna utengenezaji wa boti mpya za abiria tena za kisasa.

(a) Je, ni vigezo gani vilivyotumika kuziandaa boti hizo.

(b) Je, boti hizo zitagharimu bei gani.

(c) Je, ni lini boti hizo zinategemewa kumaliza na kuja Zanzibar.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar:

Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali na kuweka masharti bora ndani yake - Kusomwa kwa Mara ya Pili.

Waziri wa Fedha:

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Chuo cha Fedha Zanzibar, Kuweka Masharti ya Utoaji wa Elimu katika Fani za Biashara na Fedha na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa Mara ya Pili.

Zanzibar,
27 Novemba, 2026.

(Hassan A. Haji)
KATIBU,
BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR.